SHUGHULI ZA KISWAHILI
G3 KAZI YA ZIADA

ALAMA	
KIWANGO	
HISIA KUTOKA KWA MWALIMU	

1. UFAHAMU (Alama 10)

1. Soma hadithi kisha ujibu maswali yafuatayo. (alama 5)

Bi. Musa ana duka. Yeye huanza shughuli zake mapema ili wateja wake wampate dukani. Katika duka lake ameweka bei kwenye bidhaa na pia bidhaa zote zimepangwa kwenye rafu. Yeye hupima bidhaa zake kwa kutumia ratili. Bidhaa ambazo Bi. Musa huuza ni kama maziwa, mikate, mchele, sukari na chumvi. Bi. Musa huwakaribisha wateja wake vizuri.

a. Bi. Musa ana nini?

_____

b. Yeye huanza shughuli zake saa ngapi?

_____

c. Bidhaa zimepangwa wapi?

_____

d. Andika vitu viwili ambavyo Bi. Musa huuza. (alama 2)

_____

2. Soma hadithi kisha ujibu maswali yafuatayo. (Alama 5)

Bwana na Bi. Juma ni wakulima. Shambani mwao kuna mifugo na mimea ya aina tofauti. Bwana Juma hulima shamba lake kwa kutumia trekta. Wakati wa kupalilia wao hufanya kazi na watoto wao. Bwana Juma hutegemea shamba lake kwa mahitaji yake yote.

a. Bwana Juma hufanya kazi gani? (alama 1)

_____

b. Kwenye shamba lao kuna nini? (alama 2)

_____

c. Yeye hutumia nini kulima? (alama 1)

_____

d. Ni nani huwasaidia kupalilia? (alama 1)

_____

2. SARUFI (Alama 15)

1. Tumia kimilikishi sahihi kujaza pengo. (alama 5)

langu, yake, wako, chake

a. Mkoba _____utaanguka.

b. Baba _____alimpeleka shuleni.

c. Jino _____linauma.